UTT AMIS

Asset Management and Investor Services

# MFUKO WA WATOTO (WATOTO FUND)

Watoto Fund

Faraja kwa Watoto

# TAARIFA FUPI YA HESABU

## KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2015

Watoto Fund

Faraja kwa Watoto

**Taarifa ya Mwenyekiti**



Ndugu Wawekezaji

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Ninayo furaha kuwakaribisheni nyote kwenye Mkutano Mkuu wa Saba (7) wa Mwaka wa Mfuko wa Watoto. Ni imani yangu kuwa mmekuwa mkifuatilia maendeleo na mafanikio ya mfuko huu kupitia vyombo mbalimbali vya habari, ikijumuisha tovuti ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS. Nimatumaini yangu pia kuwa mmepokea taarifa za mfuko huu kwa kipindi cha mwaka huu ulioishia tarehe 30 Juni 2015 nakuzichambua kwa kina. Ndugu wawekezaji, ninayo furaha kuwajulisha kuwa pato la Mfuko kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015 limekuwa zuri kiasi cha kuwa juu ya kigezo linganishi (Benchmark) na wakati huohuo Mfuko umezidi kukua kwa maana ya rasilimali na idadi ya wawekezaji baada ya kuvutia wawekezaji wapya. Hii imetokana na imani iliyojengwa na Kampuni ya Uwekezaji ya UTT kwa wawekezaji pamoja na ongezeko la elimu kwa wawekezaji kuhusu faida za mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

**Hali ya Uchumi pamoja na utendaji wa Masoko ya Fedha.**

Pamoja na wasiwasi na kutokuwepo kwa uhakika wa hali ya kiuchumi na utendaji wa masoko uliosababishwa na uwepo wa Uchaguzi Mkuu na changamoto zinginezo, pato la ndani la Taifa limeendelea kukua kwa kiwango cha asilimia 7.2. Ndugu wawekezaji, takwimu hizi chanya ni za ndani lakini pia zimethibitishwa na taasisi huru za kimataifa ikiwemo Umoja wa Mataifa.

Taarifa ya uwekezaji Duniani (the World Investment Report) ya mwaka 2015 iliyotolewa kwenye Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Maendeleo (UNCTAD) inaonyesha kuwa Tanzania iliongoza kuwa nchi iliyopata uwekezaji toka nje kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, kwa uwekezaji uliofikia kiasi cha dola za kimarekani bilioni 2.142 kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Hii inaonyesha imani ya wawekezaji wa nje kwa nchi yetu pamoja na mazingira bora ya uwekezaji yapatikanayo nchini. Kuhusu Soko la Mitaji, hali ya maendeleo na ukuaji wa soko hilo umeendelea kuwa mzuri. Hata hivyo, pamoja na kuwa huwa kunakuwepo na mdororo wa ukuaji wa Masoko ya mitaji hasa katika vipindi vya uchaguzi, ni vema tukaelewa kwamba, wawekezaji wa nje wameendelea kufanya miamala mikubwa katika soko la hisa la Dar es salaam.

Kwa kipindi cha miezi mitatu ya mwisho wa mwaka (Aprili-Juni 2005), wawekezaji wa nje walifanya miamala ya ununuzi wa Hisa/Dhamana ya asilimia 86 na miamala ya uuzaji wa Hisa/Dhamana ya asilimia 41 katika Soko la Hisa la Dar es salaam.

Ndugu wawekezaji, Uimara wa uchumi ni muhimu katika utendaji wa masoko ya fedha, utendaji wa Kampuni ya uwekezaji ya UTT AMIS pamoja na mifuko yake. Katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2015, Tanzania imeshuhudia kushuka kwa thamani ya shilingi kwa kiwango cha asilimia 20. Pamoja na kwamba hakukuwa na athali za moja kwa moja kwa Mfuko wa Watoto, kuongezeka kwa kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni umekuwa na athali kwa utendaji wa makampuni hasa yenye dhima kubwa zilizo katika fedha za kigeni. Kushuka kwa thamani ya pesa za kitanzania kumetokana na kupanda kwa thamani ya dola za kimarekani katika soko la kimataifa pamoja na kiwango kidogo cha fedha za kigeni ziingiazo katika masoko ya ndani

Napenda niwashukuru wadau wote pamoja na Serikali kwa kuendelea kuimarisha hali ya uchumi kwa ujumla wake.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2015, Mfumuko wa bei umeendelea kudhibitiwa na kubaki katika kiwango cha asilimia 6.1.

Bila kujali kushuka kwa viwango vya riba ukilinganisha na mwaka wa fedha ulioishia Juni 2014, viwango vya riba halisi kwa mwaka ulioishia Juni 2015 vimebakia kuwa asilimia 13 ambayo imesababisha kuendelea kuwa na pato chanya katika Nyanja mbalimbali za uwekezaji.

**Ukuaji wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja na Mafanikio Mengineyo**

Kwa kipindi cha mwaka uliopita, Mifuko yote mitano ya uwekezaji wa pamoja imekua kwa jumla ya kiwango cha asilimia 34.36 kutoka kiasi cha shilingi za kitanzania 178.7 bilioni (mwaka 2014) mpaka shilingi za kitanzania 240.1 (mwaka 2015). Idadi ya wawekezaji pia imeendelea kukua nakufikia 118,811 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2015. Kwa Mfuko wa Watoto pekee umekua kwa kiwango cha asilimia 44 kutoka shilingi za kitanzania 1.85 bilioni (Mwaka 2014) mpaka shilingi za kitanzania 2.467 bilioni (Mwaka 2015). Kiwango hiki cha kuvutia cha ukuaji wa mfuko kimetokana na juhudi za makusudi za utoaji wa elimu kuhusu faida za Mfuko, utendaji mzuri wa masoko ya fedha, utendaji na maamzi sahihi ya uwekezaji yanayofanywa na Meneja wa Mfuko (yaani Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS) pamoja na kuungwa mkono na wadau mbalimbali katika uwekezaji.

Kama nilivyodokeza katika mkutano mkuu wa mwaka uliopita, ningependa kuwapa taarifa ya maendeleo ya utendaji ya Meneja wa Mfuko katika Nyanja mbalimbali pamoja na Tuzo ambayo Meneja wa Mifuko amepokea kwa kipindi cha mwaka 2015:

(i) *Kuboreshwa kwa Mifumo ya Mawasiliano na Habari (Tehama)*

Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS inaendelea na miradi mbalimbali ya kuboresha Mifumo ya Mawasiliano, Habari na Tekinolojia (Tehama) ikiwa na lengo la kuimarisha shughuli zake za

uendeshaji. Miradi hii inajumuisha kupata wadau wa kuendesha mifumo mipya, ununuzi wa vifaa vipya, mafunzo kwa wafanyakazi pamoja na uimarishaji wa miundombinu kwa ujumla.

Mara baada ya kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hii ndani ya kipindi cha miezi michache ijayo, wawekezaji wataweza kufanya miamala ya uwekezaji kwa urahisi na uhakika zaidi kupitia simu zao za mkononi. Vilevile mfumo mzima wa shughuli za uwekezaji na rasilimali zake, ikiwemo kumbukumbu za mahesabu zitakuwa zikifanywa kwa kiwango cha juu cha mifumo ya kompyuta (High level of Automation).

(ii) *Elimu ya Uwekezaji Kwa Umma Kuhusu Faida za Uwekezaji wa Pamoja.*

Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS imeendelea na utoaji wa elimu kwa umma kuhusu faida ya kuwekeza katika Mifuko ya uwekezaji wa pamoja. Elimu hii imekuwa na manufaa kwani imethibitishwa na ongezeko la mauzo ya vipande.

(iii) *Tuzo ya Meneja Bora wa Usimamizi wa Rasilimali na Uwekezaji Tanzania (Best Fund Manager in Tanzania) kwa Mwaka 2015*

Ni furaha yangu kuwajulisha kuwa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS ilipokea Tuzo ya Meneja Bora wa Usimamizi wa Rasilimali na Uwekezaji Tanzania kwa Kipindi cha mwaka 2015 kutoka Kampuni ya Kimataifa ya Capital Finance International (CFI). Kampuni hii hutoa taarifa, uchambuzi na tathimini kuhusu masoko ulimwenguni kote.

Kwa kutumia tovuti yake pamoja na majarida mbalimbali yanayochapishwa na kampuni hii, CFI huzingatia vigezo vya kiuchumi, kisiasa na kibiashara vinavyoathili masoko ili kutambua Eneo, Sekta na Kampuni zitakazofanikiwa. Ili kukidhi viwango vya kupata Tuzo hii, CFI hutathimini Kampuni au Taasisi mbalimbali kwa kuzingatia vigezo kama Uthibiti wa Hatari (Risk Management), Uwazi, Utedendaji wa Rasilimali chini ya uangalizi wa meneja, Utekelezaji wa sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za mamlaka tofauti, Utawala Bora, Ubunifu, Ubora wa Mawasiliano, Uimamara na Weledi wa Timu ya Uwekezaji katika suala zima la uwekezaji, Mawasiliano katika Nyanja za hatari za uwekezaji , Utendaji katika Nyanja za kifedha na uimara katika uteuzi. Tuzo hii hutoa mrejesho kuwa taasisi iliyopata tuzo inafanya vyema katika Nyanja hizo.

Ningependa kuipongeza Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Kampuni ya UTT AMIS na Wadau wote kwa mafanikio hayo.

**Changamoto**

Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, ikiwa ni Taasisi ya Kifedha tunatambua kuwa utendaji na mwelekeo wake pamoja na mifuko kwa siku za usoni unategemea na jinsi tunavoshughulikia usimamizi wa hatari (Risk Management) mbalimbali za uwekezaji pamoja na changamoto zinginezo. Uhitaji wa huduma zinazozingatia mifumo ya kompyuta na tekinolojia nyinginezo ni changamoto ambayo tumeendelea kupambana nayo kwa nguvu zote hadi tutakapokuwa tumeikamilisha kwa kiwango cha kuridhisha. Pia tunaendelea kujenga uwezo wa ndani kwa wafanyakazi pamoja na mazingira ya kazi kiujumla. Tunanuia kujenga uwezo maalumu katika Nyanja mbalimbali ndani ya taasisi kwa kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa kiwango cha kimataifa. Tutaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu mifuko yetu ili washiriki katika uwekezaji na kukuza uchumi wao binafsi na wa taifa letu kwa ujumla.

**Matarajio kwa kipindi cha Mwaka 2015/16**

Katika kutekeleza mipango yake ya siku zijazo, Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS itaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano 2014/19 ambao unatoa vipaumbele na mwelekeo wa Kampuni pamoja na Mifuko yake.

Moja kati ya kazi muhimu katika mpango Mkakati huo ni pamoja na kuimarisha huduma kwa wateja nakuwafikia wawekezaji wengi kadiri inavyowezekana. Katika kutekeleza hili, Kampuni inatekeleza miradi miwili ya kuboresha Mifumo ya Habari na Mawasiliano (Tehama), miundombinu ya huduma kwa wateja na usimamizi wa rasilimali za wawekezaji. Miradi hii imepangwa kuwa imekamilika ifikapo au kabla ya tarehe 30 Juni 2016.

Kampuni ya Uwekezaji ya UTT itaendelea kufuatilia kwa ukaribu soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kubaini fursa muhimu ambazo zitawanufaisha wawekezaji wote. Pia tutaendelea kutekeleza shughuli zingine kama zilivyoainishwa kwenye Mpango Mkakati.

Kutokana na jinsi Soko la Mitaji linavyoendelea kuimarika, Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS ina dhamira ya kuendelea kutoa huduma za kiwango cha kimataifa pamoja na kuimarisha uwezo wa ndani ili kutoa huduma za kiushindani katika ukanda huu. Hii ndiyo sababu kubwa iliyotupelekea kutoa vipaumbele vya kuendelea kujenga uwezo kwa watumishi wetu na miundombinu mingine kwa kipindi chote cha mwaka ulioishia tarehe 30 June 2015.

Ieleweke kuwa, vipaumbele hivi vitasaidia katika kulinda uwekezaji wenu pamoja na kutoa pato zuri kwa kipindi cha muda wa kati na muda mrefu.

**Shukrani.**

Kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, imekuwa ikipata mrejesho mzuri wa huduma zake pamoja na kuungwa mkono na wadau mbalimbali. Kama ilivyokuwa kawaida, bado tunahitaji kuungwa mkono zaidi na wawekezaji wetu, watunga sera,

mamlaka za usimamizi wa shughuli mbalimbali na wadau wote kwa ujumla. Shukrani maalumu ziwafikie Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana kwa kutuunga mkono katika mambo yote yaliyo ndani ya uwezo wake kisheria.

Mwisho, kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ningependa kuwashukuru ninyi wawekezaji wetu wote, Serikali yetu, mamlaka mbalimbali za usimamizi, Watunga Sera, Wajumbe wenzangu wa Bodi pamoja na Wadau wote kwa kutuunga mkono. Vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza Menejimenti na Wafanyakazi wote wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS kwa kazi nzuri wanayoifanya na niwaombe waendelee na utendaji mzuri kwa kipindi cha miaka ijayo.

Mimi binafsi kama Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi, nawasilisha taarifa hii kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS ambao kwa umoja wao wamechangia matokeo mazuri ya uwekezaji wenu. Tafadhali nawaombeni msisite kuwasiliana nasi panapo kuwa na jambo lolote ikiwemo maswali, ushauri au mapendekezo yoyote ambayo mtapenda kutushirikisha.

**Prof. Joseph Kuzilwa**
Mwenyekiti wa Bodi

## MFUKO WA UWEKEZAJI WA WATOTO (WATOTO FUND) TAARIFA FUPI YA HESABU KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2015

### TAARIFA YA MWANGALIZI WA MFUKO KWA WAWEKEZAJI

Tukiwa ni waangalizi wa Mfuko wa **Watoto**, Jukumu letu ni kusimamia kwamba utendaji wa meneja wa mfuko unaendana/unazingatia waraka wa makubaliano ili kuhakikisha maslahi bora ya wenye vipande. Katika utekelezaji wa kazi hii, mwangalizi wa mfuko ana majukumu yafuatayo; Uangalizi wa mali za mfuko, kuhakikisha meneja wa mfuko anatumia njia/mbinu sahihi katika kukokotoa mahesabu ya thamani ya mfuko sambamba na mkataba wa makubaliano, na pia kuhakikisha viwango vya uwekezaji vinazingatiwa.

Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, kilichoanzia tarehe 01.07.2014 mpaka 30.06.2015, Benki ya CRDB kama mwangalizi wa mfuko wa **Watoto**, tumeendeleza uangalizi wa mwenendo wa shughuli za meneja wa mfuko, utekelezaji wake na kuangalia changamoto kwenye uwekezaji.

Kwa kuzingatia hayo, tunapenda kuwathibitishia kwamba shughuli za uwekezaji kwenye mfuko wa **Watoto** na wajibu wa meneja wa mfuko (UTT AMIS), vimeendeshwa/ vimetekelezwa kufuatana na vipengele vya waraka wa makubaliano. Tukizingatia suala la imani/ uaminifu wa wenye vipande kwenye mfuko, tunathibitisha kwamba maslahi ya wenye vipande ndani ya mfuko wa Watoto yanalindwa na kuzingatiwa ipasavyo, na meneja ameendesha mfuko kulingana na waraka wa makubaliano.

**Charles Kimei (Dk)**
CRDB Bank PLC

**Tarehe**: Oktoba 2015

### TAARIFA YA MKAGUZI WA HESABU WA MFUKO WA WATOTO (WATOTO FUND)


KPMG

**KPMG**
Shirika la Wahasibu
**Ghorofa ya 11,** Jengo la PPF
Kona ya mitaa ya Ohio na Garden
S. L. P 1160

Simu: +255-22118866
Nukushi: +255-22-2113343
Barua Pepe: info@kpmg.co.tz
Tovuti: www.kpmg.co.tz


a) Taarifa ya hesabu za mfuko zilizowasilishwa, yaani Taarifa ya Mapato na Matumizi, Urari wa Hesabu za Mfuko, Taarifa ya Mabadiliko ya Thamani ya mfuko na Taarifa ya mtiririko wa fedha ni sehemu ya taarifa kamili ya Hesabu za Mfuko iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015 na ambazo zilipitishwa na Bodi ya Wadhamini wa Mfuko Mnamo tarehe 30 Oktoba 2015 na kutiwa saini na Mwenyekiti wa Bodi na Mjumbe mmoja. Ili kupata picha kamili ya ufanisi wa Mfuko na Hesabu zake ni muhimu kuchambua taarifa kamili ya hesabu za Mfuko inayopatikana katika ofisi za Kampuni ya Uwekezaji ya UTT (UTT AMIS).

b) Taarifa kamili za Hesabu za mfuko zimekaguliwa na KPMG (Shirika la Wahasibu) na ripoti yake isiyo na kasoro juu ya hali ya Hesabu za mfuko kwa kipindi hicho imetolewa.



**M Salim Bashir**
KPMG

Tarehe : Oktoba, 2015

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI (Income statement) KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI 2015

| | 2015 TZS '000 | 2014 TZS '000 |
|---|---|---|
| Mapato yatokanayo na riba | 236,619 | 165,522 |
| Mapato mengineyo | 435,563 | 281,721 |
| **Jumla ya Mapato** | **672,182** | **447,243** |
| Gharama za uendeshaji | (66,668) | (45,431) |
| **Mapato halisi kabla ya Kodi** | **605,514** | **401,812** |
| **Kodi** | (17,339) | (14,227) |
| **Mapato halisi baada ya Kodi** | **588,175** | **387,585** |
| Mapato mengineyo | - | - |
| **Ongezeko halisi la Mfuko** | **588,175** | **387,585** |

## TAARIFA YA URARI WA HESABU ZA MFUKO (Statement of Financial Position) MNAMO TAREHE 30 JUNI 2015

| | 2015 TZS'000 | 2014 TZS'000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali za Mfuko** | | |
| Fedha Taslim | 613,320 | 486,742 |
| Akaunti za muda wenye Mabenki | 516,608 | 255,773 |
| Hati Fungani (Bonds) | 373,760 | 347,927 |
| Hisa zilizoorodheshwa | 1,181,887 | 745,352 |
| Rasilimali nyinginezo | 30,550 | 50,773 |
| **Jumla kuu ya Rasilimali** | **2,716,125** | **1,886,567** |
| | | |
| **Dhima (Liabilities)** | | |
| Kodi ya mapato | 6,072 | 4,825 |
| Dhima nyinginezo | 26,281 | 33,155 |
| **Jumla ya Dhima ya mfuko** | **32,353** | **37,980** |
| | | |
| **Thamani halisi ya mfuko** | **2,683,772** | **1,848,587** |
| | | |
| **Inawakilishwa na:** | | |
| **Thamani halisi ya mfuko** | **2,683,772** | **1,848,587** |
| | | |
| **Thamani ya Kipande kwa idadi ya Vipande** 9,726,799 (2014 – 8,780,287) | **275.92** | **210.54** |
| | | |
| Thamani ya kipande iliyotangazwa | **275.92** | **210.54** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA THAMANI YA MFUKO
## (Statement of changes in Net Assets attributable to Unit holders)
## KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2015

| | 2015<br>TZS'000 | 2014<br>TZS'000 |
|---|---|---|
| Thamani ya mfuko 1 Julai 2014 na 01 Julai 2013 | 1,848,587 | 1,311,008 |
| Mabadiliko ya thamani ya mfuko | 588,175 | 387,585 |
| | **2,436,762** | **1,698,593** |
| **Thamani ya Vipande vilivyonunuliwa na kuuzwa na wamiliki:** | | |
| Mauzo ya vipande(Sales) | 356,969 | 200,357 |
| Ununuzi wa vipande(Repurchases) | (109,959) | (50,363) |
| **Mabadiliko ya thamani ya mfuko:** | **247,010** | **149,994** |
| **Thamani halisi ya Mfuko** | **2,683,772** | **1,848,587** |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA MAPATO (Cash flows statement)
## KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2015

| | 2015<br>TZS'000 | 2014<br>TZS'000 |
|---|---|---|
| **MAPATO YATOKANAYO NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | |
| Mapato halisi yatokanayo na uendeshaji kabla ya Kodi | **605,514** | **401,812** |
| **Imerekebishwa na:** | | |
| Mapato yasiyo fedha taslimu yatokanayo na (ongezeko)/punguko la thamani ya Dhamana, Hati Fungani pamoja na Hisa | (435,563) | (273,295) |
| **Mapato halisi kabla ya marekebisho ya mtaji wa uendeshaji** | **169,951** | **128,517** |
| Kupungua / (Ongezeko) kwa riba ambayo haijapokelewa | 20,223 | (27,817) |
| Kupungua / (Ongezeko) kwa Dhima ambayo haijalipwa | (6,874) | (19,802) |
| **Fedha iliyopatikana kutoka kwenye shughuli za uendeshaji baada ya marekebisho ya mtaji** | **183,300** | **80,898** |
| Kodi iliyolipwa kwa mwaka 2014/2015 | (16,090) | (14,330) |
| Mapato yasiyo fedha taslimu yatokanayo na (ongezeko)/punguko la thamani ya Dhamana, Hati Fungani pamoja na Hisa | 435,563 | 273,295 |
| **Fedha halisi itokanayo na shughuli za uendeshaji** | **602,772** | **339,863** |
| **FEDHA KATIKA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI ULIOFANYWA NA MFUKO**: | | |
| Akaunti za muda katika mabenki | (260,835) | (233,595) |
| Hati Fungani | (25,832) | 47,463 |
| Hisa zilizoorodheshwa | (436,535) | (323,811) |
| **Fedha halisi iliyotumika katika shughuli za Uwekezaji** | **(723,202)** | **(509,943)** |
| **AMANA YA MFUKO (FINANCING ACTIVITIES)** | | |
| Michango ya wenye vipande | 356,969 | 200,357 |
| Ununuzi wa vipande ( Repurchase) | (109,959) | **(50,353)** |
| **Fedha/Amana halisi toka kwa wenye vipande** | **247,010** | **149,994** |
| **Ongezeko/(punguo) halisi la Fedha** | **126,578** | **(20,086)** |
| Salio la fedha mwanzoni mwa Mwaka | **486,742** | **506,828** |
| Salio la fedha mwishoni mwa Mwaka | **613,320** | **486,742** |

**Mkurugenzi** **Mkurugenzi**

**Tarehe**: Oktoba, 2015

# TAARIFA YA MENEJA KWA WAWEKEZAJI KUHUSU UWEKEZAJI

Mfuko wa Watoto ni mfuko wa wazi wa uwekezaji wa pamoja wenye lengo la kutoa suluhisho la kifedha kwa kufanya uwekezaji wa muda mrefu ili kukuza mtaji kwa ajili ya kuandaa elimu ya watoto wetu na maisha yao ya baadaye.mfuko una mipango miwili ya uwekezaji; (a) mpango wa elimu na (b) mpango wa kukuza mtaji
Katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Mfuko wa Watoto umepata faida maridhawa.Thamani ya kipande ilikuwa shilingi 275.92 mnamo juni 30,2015 ikilinganishwa na shilingi 210.54 mwishoni mwaka wa fedha 2013/2014.Thamani ya mfuko iliongezeka kwa asilimia 44.86 kutoka shilingi bilioni 1.85 hadi bilioni 2.68 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2014/205

**Mgawanyo wa Uwekezaji:**

Sawa na sera na taratibu za uwekezaji katika mfuko, kufikia Juni 30,2015 mgawanyo anuai wa uwekezaji rasilimali za mfuko ulikuwa kama ifuatavyo

**Kielelezo Na 1: Mgawanyo wa uwekezaji kwenye Mfuko wa Watoto hadi Juni 30,2015**




Kama inavyoonekana kwenye kielelezo na.1 hapo juu, mfuko uliwekeza kiasi cha asilimia 44 ya rasilimali yake kwenye hisa,uwekezaji kwenye amana za benki za muda maalum asilimia 41,hati fungani za serikali asilimia 12,hati fungani za mashirika asilimia 2 na amana za benki za muda mfupi asilimia 1. Fedha katika amana za benki za muda mfupi zinawekwa ili kuhakikisha hali ya ukwasi ya mfuko kwa kukidhi mahitaji ya wawekezaji wanao uza vipande vyao.

**<u>Thamani ya Mfuko na Thamani halisi ya Kipande</u>**

Mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2015 ukubwa wa mfuko na thamani halisi ya vipande imeendelea kukua vizuri.Thamani ya mfuko ilikua kutoka shilingi bilioni **1.85** mwanzoni mwa mwaka hadi kufikia shilingi bilioni **2.68** mwishoni mwa mwaka, hili ni sawa na ongezeko la asilimia **44.86**. Thamani halisi ya kipande iliongezeka kwa asilimia **30.87** kutoka shilingi **210.54** kwa kipande mwamzoni mwa mwaka hadi shilingi **275.72** mwishoni mwa mwaka wa fedha juni 30, 2015

Grafu hapa chini linaonyeshwa mwenendo wa thamani ya mfuko na thamani ya kipande kutoka Julai 2014 hadi Juni 2015

**KUANZISHWA OKTOBA 2008**

**30 JUNI 2015**

**THAMANI YA KIPANDE TSH 275.92**

**THAMANI YA MFUKO TSH 2.68 BILIONI**

**FAIDA YA MFUKO 31.05%**

**Grafu Na2: Ukuaji wa thamani ya mfuko na kipande katika mfuko wa watoto hadi juni 30,2015**




**Faida**

Katika kipindi hichi,ufanisi wa Mfuko wa Watoto katika kutoa faida kwa wawekezaji wake umekuwa wa kuridhisha.Toka Julai,2014 hadi Juni,2015 mfuko ulipata faida ya asilimia 31.47 ambayo ni ya kuridhisha ukilinganisha na sehemu nyingine katika masoko ya fedha.Jedwali hapa chini linaonyesha faida ya mfuko katika vipindi mbalimbali hadi juni 30, 2015.

**Jedwali Na 1: Faida ya Mfuko wa Watoto hadi Juni 30,2015**

| Faida ya Mfuko(%) kwa Mwaka, hadi Juni 30,2015 | Kiwango |
|---|---|
| Tangu kuanzishwa hadi 30 Juni 2015 | 16.90% |
| Miaka 5 iliyopita | 19.61% |
| Miaka 4 iliyopita | 21.33% |
| Miaka 3 iliyopita | 24.36% |
| Miaka 2 iliyopita | 31.24% |
| Mwaka 1 uliopita | 31.47% |

**Jedwali Na: Ulinganishaji wa Dhamana katika masoko ya fedha**

| BIDHAA | MWISHO WA ROBO YA MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Jun-14 | Sept-14 | Dec-14 | Mar-15 | Jun-15 |
| Dhamana za serikali za siku 182 | 12.77 | 13.16 | 15.22 | 9.10 | 11.47 |
| Dhamana za serikali kwa ujumla (%) | 12.51 | 12.62 | 15.73 | 9.04 | 10.04 |
| Hati fungani za miaka 2 (%) | 13.8 | 14.12 | 14.83 | 8.47 | 14.01 |
| Akaunti za akiba (%) | 3.12 | 3.10 | 3.12 | 3.42 | 3.52 |
| Amana za mabenki za miezi 12 | 11.08 | 10.52 | 10.66 | 11.00 | 10.78 |
| Viwango vya riba kwa makubaliano | 10.83 | 9.82 | 10.70 | 9.35 | 8.62 |

**Chanzo: Benki kuu ya Tanzania**

Ingawa uwekezaji katika dhamana za serikali hauna uwezekano wa kupata hasara,ili kulinganisha na faida za uwekezaji katika Mfuko wa Watoto,mambo kadhaa yanapaswa yazingatiwe:

- Viwango vya riba vilivyoonyeshwa hapo juu ni kabla ya kodi ya zuio ya 10%(w/tax),wakati mapato ya Mfuko wa Watoto ni baada ya kodi ya zuio ya 10% (w/tax)
- Suala jingine la kuzingatia ni kuwa Mfuko wa Watoto unaruhusu wanachama kuuza vipande vyake wakati wowote sawa na masharti

ya mfuko,hivyo kumpa fursa ya kupata fedha taslimu pindi anapozihitaji.

- Sehemu nyingine za uwekezaji huwa zina muda maalum wa uwekezaji na kama kuna uhitaji wa haraka atalazimika kupokea sehemu ya pato(discounted)hivyo kupata hasara.
- Faida ya mwaka mmoja iliyoainishwa hapo juu hupatikana kwa wawekezaji wakubwa na taasisi ambao huwekeza kiasi cha kuanzia shilingi milioni 500 na kuendelea wakati faida ya Mfuko wa Watoto hupatikana kwa wawekezaji wote(wadogo,wakati na wakubwa)

Mfuko wa watoto umekuwa suluhisho sahihi kwa wazazi na walezi kuanza mapema kuaanda elimu ya sekondari hadi chuo kikuu huku wakikuza mitaji yao kwa faida shindani zaidi.

**Mwenendo wa Uchumi:**

Kwa takwimu zilizotolewa na Taasisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) zinaonyesha uzalishaji ndani ya nchi umekua kwa asilimia 7.9 kwa kipindi kilichoishia mwezi wa sita mwaka 2015. Ukuaji huu wa uchumi ndani ya nchi umebakia kuwa imara. Mwaka 2014/2015 uchumi ulikua kwa asilimia 7.0 ingawa ni mdogo zaidi ukilinganisha na asilimia 7.3 kwa mwaka uliopita. Ukuaji wa uchumi wa ndani ulichangiwa na Hali nzuri ya hewa na uongezekaji wa shughuli za ujenzi wa miundo mbinu. Ukuaji huu wa uchumi wenye kufurahisha pia umechangiwa na biashara imara ya jumla na rejareja, usafirishaji, usindikaji na Shughuli za viwanda, ambapo shughuli za ujenzi zimechangia kwa asilimia 14.1, asilimia 12.5 usafirishaji na usindikaji, asilimia 10.8 shughuli za kifedha na bima huku Biashara za jumla na rejare zikichangia kwa asilimia 10.0

Kwa sasa shughuli zinazoendelea za uwekezaji kwenye miundo mbinu, ukuaji wa sekta binafsi na sekta za umma, uboreshwaji kwa sekta zetu za nje ya nchi kama soko la dunia linavyozidi kuimarika kutapelekea uchumi wa nchi yetu kuwa imara zaidi na kukadiriwa kukua kwa asilimia 7.2 kwa mwaka 2015 na hata baadae.

**Sekta ya Benki:**

Sekta za kibenki zimeendelea kukua na kufanya vizuri hususani amana za wateja na mali za benki, ukuaji huo umefanikiwa kutokana na mazingira mazuri ya ukuaji uchumi.

Jumla ya mali ilikua kwa asilimia 11.4 na kufikia kiasi cha fedha za kitanzania shilingi bilioni 23,479.1 kwa mwaka ulioishia mwezi machi 2015, huku amana za wateja zikikua kwa asilimia 13.9 hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 17,904.7. Aina zote za mikopo katika mabenki imefikia asilimia 53.0 ya mali zote. Vilevile Ukuaji katika sekta hii umechangiwa na kufunguliwa matawi, kuwepo kwa mawakala, na kuongezeka kwa uhusiano kati ya benki na mashirika ya kijamii ya kuweka na kukopa (SACCOS) pamoja na kampuni za mitandao ya simu.

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa nne mwaka 2015, benki kuu ilifanikiwa kutoa leseni kwa benki mbalimbali ili zitoe huduma kwa njia ya mawakala. Jumla ya mikataba 2,013 ilisainiwa na mawakala na kupelekea kuongezeka kwa miamala ya dhamana za wateja kufikia kiasi cha fedha za kitanzania shilingi bilioni 503.10 huku miamala 272,282 ya kutoa pesa yenye thamani ya shilingi bilioni 75.50. Miamala ya malipo kwa njia ya simu imeendelea kukua na kukadiriwa kufikia miamala yenye thamani kwa wastani wa shilingi bilioni 116.8 kwa siku.

Ukuaji huo unaashiria teknolojia bora na mifumo ya ukopeshaji iliyopo ambayo imeongeza utumiaji wa huduma za kifedha kwa gharama ndogo zaidi. Taasisi za kibenki zimeendelea kuwa imara na zenye uhakika kama inavyoonyeshwa na viashiria vilivyopo vya kifedha.

**Mfumuko wa Bei:**

Mfumuko wa bei umeshuka hadi kufikia 6.1 mwezi juni mwaka 2015. Mfumuko wa bei ulibakia imara na kwa kiwango cha chini huku kushuka kwa bei za vyakula, gharama za umeme na uzalishaji na bei za mafuta katitka soko la dunia vikielezewa kua ni visababishi juu ya kuporomoka kwa mfumuko huo wa bei.

Mfumuko wa bei mbali na vyakula ni asilimia 1.3 kidogo ukilinganisha na asilimia 4.6. Pia mfumuko wa vyakula na vinywaji visivyo na kilevi ilikua asilimia 8.6 ukilinganisha na asilimia 8.1 mwaka uliopita.

**Jedwali I: Kasi ya Mfumuko wa Jumla wa bei kwa kipindi Kilichoanzia Julai 2014 mpaka Juni 2015**

| Tarehe | Julai-14 | Ago-14 | Sept-14 | Oct-14 | Nov-14 | Dis-14 | Jan-15 | Feb-15 | Mac-15 | Apr-15 | May-15 | Juni-15 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kasi ya Mfumuko wa jumla wa bei (%) | 6.5 | 6.7 | 6.6 | 5.9 | 5.8 | 4.8 | 4.0 | 4.2 | 4.3 | 4.5 | 5.3 | 6.1 |

## Dhamana za Serikali:

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Benki Kuu ya Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitangaza zabuni za dhamana za muda mfupi za serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 2,495.00 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia ambapo zabuni zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 3,645.00. Mahitaji ya soko yalikuwa na thamani ya shilingi bilioni 4,899.43 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia mahitaji yalikuwa shilingi bilioni 5,346.50, lakini pamoja na hali kuwa hivyo serikali ilikubali maombi yenye thamani ya shilingi bilioni 3,339.52 ikiwa chini ikilinganishwa na mwaka ulio tangulia ambapo serikali ilikubali maombi yenye thamani ya shilingi bilioni 3,389.70

Kwa ujumla riba za Dhamana za Serikali zilishuka kutoka wastani wa asilimia 12.65 Juni 2014 hadi asilimia 10.04 Juni 2015.

Vilevile, Benki Kuu ilitangaza zabuni kwa dhamana za muda mrefu za serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 1,284.00 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia ambapo zabuni zilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 832.25. Serikali ilikubali maombi yenye thamani ya shilingi bilioni 1,072.49 ikiwa juu ikilinganishwa na mwaka ulio tangulia ambapo serikali ilikubali maombi yenye thamani ya shilingi bilioni 751.72.

## Viwango vya Riba:

Katika kipindi kinachoishia Juni 2015, Viwango vya riba katika benki za biashara vilishuka. Kiujumla riba katika amana za mabenki zilipanda hadi kuifikia wastani wa asilimia 8.89 Juni 2015 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.12 ilivyokuwa mwezi juni mwaka 2014, wakati kiujumla riba za mikopo zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 16.07 kutoka asilimia 16.43 mwaka uliopita.

Kwa upande mwingine riba za amana za miezi 12 zilipungua kidogo kutoka wastani wa asilimia 10.71 juni 2014 mpaka wastani wa asilimia 10.54 mwishoni mwezi Juni 2015.

Katika kipindi hicho hicho viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja ziliongezeka kufikia asilimia 14.65 mwezi Juni 2015 ukilinganisha na asilimia 14.17 ya mwezi Juni 2014.

Kwa hali hiyo, utofauti baina ya riba za amana ya mwaka mmoja na riba za mikopo ya muda mfupi iliongezeka hadi kufikia asilimia 4.11 toka asilimia 3.59 mwezi mei mwaka 2015.

## Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni:

Katika kipindi cha mwaka fedha 2014/2015, shilingi ya Kitanzania imeshuka thamani kufikia wastani wa shilingi 1,951.7 kutoka wastani wa shilingi 1,647.70 mwaka jana kwa kila dola ya kimarekani. Hali ambayo imeashiria punguzo la thamani kwa asilimia 18.40 kwa mwaka na ni punguzo kubwa la anguko la thamani kutokea hivi karibuni.

Shughuli za uwekezaji zimeathirika sana kutokana na kuporomoka kwa thamani ya fedha ya kitanzania dhidi ya fedha ya kimarekani kutokana na matokeo hasi kwenye marejesho.
Kushuka kwa thamani ya shilingi kwa dola moja ya kimarekani kumesababishwa na sababu za nje na ndani ya nchi. Kwa kipindi cha

pili cha nusu mwaka 2014 dola ya kimarekani iliimarika sana dhidi ya fedha zingine duniani kote hali ambayo ilisababishwa na kufanya vizuri kwa uchumi nchini marekani, hali hii pia ilisababisha uhitaji mwingi wa dola ya kimarekani kuongezeka kwani wawekezaji wengi hupenda kuwekeza kwenye uchumi wa marekani.

Poromoko la thamani ya fedha ya kitanzania limeongezeka kutoka asilimia 2.5 mwezi julai mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 9.0 mwezi machi mwaka 2015, mwenendo huo pia umeonekana baina ya fedha zingine dunia dhidi ya dola moja ya kimarekani.

Kutoka mwezi wa nne mwaka 2015 na kuendelea, poromoko la thamani ya fedha ya kitanzania dhidi ya dola moja ya kimarekani imesababishwa na sababu za ndani ya nchi hususani kupungua kwa mapato ya mauzo ya nje ya nchi kwa bidhaa kama dhahabu na pamba.

Kwa upande wa pili pia kupungua kwa mapato katika sekta za utalii, kilimo na kufanyika kwa malipo ya gawio kwa kiwango kikubwa kwa wawekezaji wa nje. Pia ucheleweshwaji wa mgawanyo wa programu saidizi za bajeti na mikopo, zimechochea kisaikolojia kupungua kwa viwango vya kubadilisha fedha za kigeni hali ambayo imesababisha kuongezeka kwa mikataba ya muda maalumu sokoni.

Tabia hii imechangia sana kasi ya kushuka thamani ya fedha ya kitanzania kwa kipindi cha mwisho wa mwaka wa fedha 2014/ 2015.

**Hisa zilizoorodheshwa:**

Katika Mwaka huu wa fedha 2014/2015, tumeshuhudia kwa ujumla bei za hisa zikifanya vizuri na kuongezeka katika soko la hisa la Dar es Salaam (DSE), ukubwa wa soko la hisa kwa ujumla uliongezeka kwa thamani ya Tsh Trilioni 4.8 na Tsh Trilioni 2.4 kwa ukubwa wa soko la hisa ndani ya nchi. Ikiripotiwa mnamo tarehe 30 mwezi wa sita mwaka 2015 ukubwa wa soko la hisa lilifikia Tsh trilioni 23.721 wakati ukubwa wa soko la mitaji ndani ya nchi ukitajwa kufikia Tsh Trilioni 9.927.

Index za jumla na ndani ya Soko la hisa la Dar es Salaam (DSE), zimeripotiwa kuongezeka na kufanya vizuri zaidi kwa takribani asilimia 25.50 kwa upande wa soko la jumla na asilimia 32.00 kwa index za soko la ndani. Ongezeko hilo limesababishwa na kufanya vizuri kwa sekta za viwanda na sekta washirika za viwanda pamoja na sekta za biashara na huduma za kifedha.

Jumla ya mauzo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 mwezi juni mwaka 2015 yameongezeka na kufikia kiasi cha Tsh bilioni 878 ukilinganisha na Tsh bilioni 274 mauzo yaliyolipotiwa mwaka jana. Huku kiwango cha miamala ya hisa ikiongezeka kwa asilimia 6.0 toka hisa milioni 258 hadi hisa milioni 274

UTT AMIS inapenda kuwahakikishia wawekezaji wake kuwa itaendelea kubuni na kuvumbua mianya stahiri ya uwekezaji kadri inavyojitokeza katika soko, ili kuongeza mapato na faida. Lengo letu ni kuvuka matarajio ya wawekezaji na kuwawezesha kwa ajili ya maendeleo yao na taifa kwa jumla.

**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa UTT AMIS wanawatakia nyote msimu wa sikuku uliojaa furaha tele na Kheri ya Mwaka Mpya 2016**

**Faraja kwa Watoto**

UTT AMIS
Asset Management and Investor Services

# Mfuko Wa Watoto
# Faraja kwa Watoto!

## Mifuko Mingine ya Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS


Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi:
**Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS**
Jengo la Sukari, Ghorofa ya Pili,
S. L. P. 14825 Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 2128460 Nukushi: +255 22 2137593,
Simu ya Bure (vodacom kwa Vodacom) 0754 800 455, 0754 800 544,
0715 800 455/ 0715 800 544(Tigo), 0782 800455(Airtel)

Barua pepe: uwekezaji@utt-tz.org Tovuti: www.utt-tz.org